Pittsburgh Public Schools
Students first
*Always, in all ways.*

Margaret Rudolph,
Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu

341 South Bellefield Avenue
Pittsburgh, PA 15213

mrudolph1@pghschools.org
412-529-4357

Septemba 12, 2023

Katika Shule za Umma za Pittsburgh (PPS), tunajivunia sana walimu na wasaidizi wetu wa walimu na kazi wanayofanya kila siku ili kuwasaidia wanafunzi wetu kufaulu. Kama mzazi, una haki chini ya Sheria ya Kuhakikisha kuwa Kila Mwanafunzi Anafaulu (ESSA), ya kuomba taarifa kuhusu sifa za walimu na wasaidizi wa walimu wanaofundisha mtoto wako, pamoja na taarifa kuhusu tathmini.

**Sifa za Walimu na Wasaidizi wa Walimu**
Chini ya miongozo ya ESSA, wazazi wanaweza kuomba taarifa ifuatayo:

- Je, mwalimu wa mtoto wangu amepewa leseni na Idara ya Elimu ya Pennsylvania ya kufundisha wanafunzi wa madarasa na masomo anayofundisha?
- Je, mwalimu wa mtoto wangu anafundisha kwa kutumia cheti cha dharura au cheti kingine cha muda?
- Je, mwalimu wa mtoto wangu ana digrii au vyeti gani vingine vya elimu ya juu?
- Je, mtoto wangu anapokea huduma kutoka kwa wasaidizi wa walimu na ikiwa ndivyo, je, sifa zao ni zipi?

**Taarifa ya Tathmini**
Taarifa ya Tathmini ya Wilaya kwa sasa inapatikana mtandaoni kwa www.pghschools.org/assessment. Hata hivyo, wazazi/walezi wanaweza pia kuomba taarifa zifuatazo kuhusu tathmini:

- Mada iliyojaribiwa/kutathminiwa
- Sababu ya kufanya tathmini
- Marejeleo ya mahitaji
- Muda ambao wanafunzi watafanya mtihani
- Jinsi na wakati ambapo wazazi watapata matokeo
- Taratibu za kusema kuwa hutaki mwanao afanye tathmini
- Sera za wilaya kuhusu kufanya tathmini

Ili uombe taarifa iliyo hapo juu, tafadhali wasilisha ombi lililoandikwa kwa Laini ya Moja kwa Moja ya Mzazi, katika anwani ya Pittsburgh Public Schools Service Center, 1305 Muriel Street, Pittsburgh, PA 15203. Tafadhali jumuisha jina, shule na darasa la mtoto wako pamoja na nambari ya simu tunayoweza kutumia kuwasiliana nawe kati ya saa 8:00 asubuhi na 4:30 jioni. Unaweza pia kutuma ombi lako kwa kuwasiliana na Timu yetu kwa Laini ya Moja kwa Moja ya Mzazi namba ni
412-529-HELP (4359).

Katika PPS, tumejitolea kuhakikisha kwamba mtoto wako anapokea mafundisho ya hali ya juu ili ahitimu akiwa tayari kwa chuo kikuu, kufanya kazi na kufanikiwa maishani.

Kwa Dhati,

Margaret Rudolph
Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu

www.pghschools.org
Laini ya Moja kwa Moja ya Mzazi:

Shule za Umma za Pittsburgh hazibagui kwa msingi wa mbari, rangi, umri, imani, dini, jinsia (ikiwemo utambulisho au maoni ya kijinsia), jinsia wanayovutiwa nayo kimapenzi, ukoo, asili ya kitaifa, hali ya ndoa, ujauzito au ulemavu katika mipango, shughuli au ajira zake na hutoa fursa sawa kwa makundi maalumu ya vijana yaliyoteuliwa. Maswali yanaweza kuelekezwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Huduma za Wanafunzi katika anwani ya 341 S. Bellefield Avenue, Pittsburgh, PA 15213 au (412) 529-HELP (4357).